Wazazi na Walezi wapendwa,

Mtoto wako atakuwa akitembelea Kituo cha Historia Asili ya Mlima Sandia (Sandia Mountain Natural History Center, SMNHC) kwa ajili ya Mpango wa Safari ya Kimasomo ya Ikolojia mnamo _____.

Sehemu kubwa ya siku itatumika kwa matembezi ya wastani ya maili 2 kupitia msitu, kwenye konde la majani, na kupanda na kushuka milima yenye miamba. Wanafunzi watakuwa wakijifunza kuhusu mfumo wa mazingira ya Milima Sandia huku wakishiriki katika shughuli za nje zilizoundwa kushirikisha watoto katika sayansi.

Mtoto wako atahitaji kubeba:
• Chakula cha Mchana na Maji
• Daftari na penseli
• Mkoba

Jiandae kwa ajili ya safari yako:
• Angalia ripoti ya hali ya hewa ya Cedar Crest
• Vaa vizuri kulingana na hali ya hewa inayotarajiwa
• Krimu ya kukinga jua

Mtoto anapaswa kuvaa:
• Viatu vya kutembea vizuri na vilivyo imara (hakuna Crocs, makubazi, au patipati)
• Fulana, koti, na/au koti la mvua
• Kofia ya jua na/au kofia yenye joto na glavu, inapohitajika

SMNHC, iko mashariki mwa Albuquerque huko Cedar Crest, iko kwenye ekari 128 za msitu wa piñon-juniper, karibu na Msitu wa Kitaifa wa Cibola, na inamilikiwa na APS kwa ushirikiano na Makumbusho ya New Mexico ya Historia na Sayansi Asili.

Kwa maelezo zaidi kuhusu SMNHC, tafadhali tembelea www.aps.edu/smnhc